



sumu ya nafaka zilizooza




kuku




ng'ombe



mayai



maziwa



chakula mezani



**Kenya Agricultural Research Institute**

S.L.P 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

**Mtayarishaji:**

Muturi, M.E.M

**Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:**

**Mkurugenzi wa Kituo,**

KARI-Embu

S.L.P.27 Embu

Simu 06820116/20873 nukulisi 068-30064

Baruapepe: kariembu@salpha.co.ke

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 31 /2008

**Shilingi Ishirini za Kenya**

**Wanyama kulishwa  
nafaka zilizooza ni  
hatari kwa afya yako**



## Utangulizi

Kuwalisha mifungo nafaka zilizooza ni jambo la kawaida hasa katika maeneo yenye mazao mengi ya nafaka.

## Kuharibika kwa nafaka ni nini?

Ni kuharibiwa kwa nafaka na vitu vyenye madhara (kama kuvu) kunakopelekea kumea kwa kuvu. Nafaka kama hizo hutoa vitu vyenye sumu.

Nafaka kama hizo zikiliwa na binadamu, sumu hiyo inaeleweka kusababisha ukuaji mbaya na hata kuleta saratani (cancer).

Nafaka hizo zikilishwa mifugo, sumu hiyo inapitishwa kupitia maziwa, nyama na mayai.



## Ni nini kinachoharibu nafaka?


- Kuvuna mbegu zikiwa na unyevu na kuweka kwenye ghala zisizo na hewa ya kutosha.
- Kuhifadhi nafaka kwenye maghala mabovu.
- Nafaka zilizohifadhiwa kupata unyevu.
- Kuharibiwa na wadudu wa nafaka, ndege na panya waharibifu.



Ghala mbovu

## Jinsi ya kuepuka viungo vya sumu katika chakula

- Zipe nafaka muda wa kutosha baada ya kuvuna.
- Zuia kuathiriwa kwa nafaka na wadudu kwani kuvu huota katika sehemu za nafaka zilizoharibiwa na wadudu.
- Nafaka yoyote yenye kuvu ichomwe au kuzikwa.
- Hifadhi nafaka kwenyae ghala zenye hewa ya kutosha na ambazo haziingizi mvua ndani.
- Jiepushe kuwalisha mifugo kwa nafaka zilizoharibika au kuzitumia kutengenezea lishe ya mifugo va nyumbani.



Usitumie nafaka zilizozwa katika chakula cha mifugo